# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 28 MACHI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, ELIYA SINDILA**

Kwa wiki inayoishia tarehe 28 Machi 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliongezeka kwa asilimia 339.18 kutoka TZS 8.49 bilioni hadi TZS 37.3 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kiliongezeka pia kwa asilimia 67.55 kutoka hisa milioni 5.04 hadi hisa 8.45 milioni

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.07 kutoka TZS 19.22 trilioni hadi TZS 19.2 trilioni.Hii nikutokana na kupungua kwa bei ya hisa za JHL na EABL, ambapo JHL ilipungua bei kwa asilimia 4.42 wakati EABL ikipingua bei kwa asilimia 4.40. Mtaji wa Soko la Ndani uliongezeka kwa asilimia 0.81, kutoka TZS 12.84 trilioni hadi TZS 12.94 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za NMB, TPCC,AFRIPRISE na CRDB.

Hisa za NMB ziliongezeka kwa TZS 150 wakati za TPCC zikiongezeka TZS 20 huku za CRDB zikiongezeka kwa TZS 10 na AFRIPRISE nazo pia ziliongezeka kwa TZS 5. CRDB iliongoza kwa idadi kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 40.7 sawa na hisa milioni 3.44 ikifuatiwa na TCC kwa asilimia 40.25 sawa na hisa milioni 3.4 na TBL ikiwa ni asilimia 16.21 sawa na hisa milioni 1.3.

TCC imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 25.2 bilioni, ambayo ni 67.65% ya mauzo yote ikifuatiwa na TBL Ikirekodi TZS 9.14 billion ambayo ni asilimia 24.52, huku CRDB ikirekodi 2.68 Billion ambayo ni sawa na asilimia 7.2 ya mauzo yote.

Shughuli za soko kwa wiki hii zimechangiwa na ushiriki mkubwa wa wawekezaji wa ndani kwa asilimia 99.99 huku ushiriki wa wawekezaji wa kigeni ukiwa ni asilimia 0.01 tu. Kwa mara ya kwanza kaunta ya NMB imefikia hatua ya kihistoria ambayo Thamani ya soko ya NMB imefikia TZS Trillion 3.Hatua hii inaashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji na utendaji thabiti wa benki.

Katika wiki kulikuwa na miamala 87 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 42.3 bilioni.

Mnada wa dhamana za Serikali za muda mfupi (Treasuty bills) wa siku 364 uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 26 Machi 2025, ulisajili zabuni 104 ambapo zabuni 25 ndizo zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 102.9 Bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA MACHI 28, 2025. KWASASA UNAWEZA KUPATA HUDUMA ZETU KUPITIA MATAWI YA SHIRIKA LA POSTA YALIYOPO NCHI NZIMA .#TUMEKUFIKIA WEKEZA CHAP CHAP. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI ELIYA SINDILA**